PRESS RELEASE

PR 24/169

# Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) Lafikia Makubaliano ya Ngazi ya Wafanyakazi na Serikali Kuhusu Mpango wa Ukopeshaji kwa ajili ya kushughulikia Changamoto za Mabadiriko ya Tabia ya Nchi (Resilience and Sustainability Facility) na Mapitio ya Tatu ya Mpango wa Ukopeshaji wa ECF (Extended Credit Facility)

**FOR IMMEDIATE RELEASE**

End-of-Mission press releases include statements of IMF staff teams that convey preliminary findings after a visit to a country. The views expressed in this statement are those of the IMF staff and do not necessarily represent the views of the IMF's Executive Board. Based on the preliminary findings of this mission, staff will prepare a report that, subject to management approval, will be presented to the IMF's Executive Board for discussion and decision.

- *Serikali ya Tanzania na IMF wamefikia makubaliano ya ngazi ya wafanyakazi kuhusu mpango wa mageuzi ya kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabia ya nchi utakaoungwa mkono na mpango wa ukopeshaji wa ECF (Resilience and Sustainability Facility) na kukamilisha mapitio ya tatu chini ya mpango wa ECF* (*Extended Credit Facility).*
- *Mpango wa RSF utasaidia juhudi za serikali katika kuendeleza mageuzi ya kimuundo na uwekezaji katika kukabiliana na hatari na changamoto za mabadiliko ya tabia ya nchi.*
- *Ukuaji wa uchumi unaimarika kutokana na athari zitokanazo na changamoto za ndani ya nchi na pia kwenye uchumi wa dunia. Vipaumbele vya sera za muda wa karibu ni pamoja na kuruhusu viwango vya ubadilishaji wa fedha kuendana na uhalisia na kubana matumizi ya serikali bila kuathiri ukuaji wa uchumi, huku matumizi ya vipaumbele kwenye huduma za kijamii yakiongezeka. Vipaumbele vya mageuzi ya muda wa kati vinaendelea kujikita katika kupata nafasi ya kuongeza matumizi ya serikali, kuboresha mfumo wa sera ya fedha kuwa wa kisasa ili kuimarisha usimamizi wa mfumo wa fedha, na kuendeleza mageuzi ya kimuundo.*

**Washington, DC-[17 Mei 2024]:** Wafanyakazi kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) wakiongozwa na Bwana Charalambos Tsangarides walifanya vikao vya majadiliano mjini Dodoma na Dar es Salaam kuanzia tarehe 2 hadi 17 Mei, 2024, ili kufanya mapitio ya tatu ya utekelezaji wa mpango wa ukopeshaji wa ECF (Extended Credit Facility). Mapitio haya endapo yataidhinishwa na Bodi Tendaji ya IMF, serikali itapokea kiasi cha SDR milioni 113.37 (takribani dola za marekani milioni 150) na hivyo kufikisha jumla ya kiasi cha SDR milioni 455.47 (takribani dola za marekani milioni 604.24) zilizokwishatolewa na IMF chini ya mpango wa ECF. Wafanyakazi pia walijadili ombi la serikali la kukopeshwa kiasi cha asilimia 150 ya kiwango cha uwekezaji cha Tanzania IMF ambazo ni sawa na SDR milioni 596.7 (takribani dola za marekani milioni 789.6) chini ya mpango wa ukopeshaji wa RSF.

Mwishoni mwa ziara yake, Bwana Tsangarides, ametoa taarifa ifuatayo:

“Ninafuraha kutangaza kwamba tumefikia makubaliano ya ngazi ya wafanyakazi kuhusu sera za kiuchumi na zinazohitajika ili kukamilisha mapitio ya tatu ya mpango wa Tanzania unaoungwa mkono na ECF, na ombi la kupata rasilimali fedha kutokana na mpango wa RSF. Bodi Tendaji ya IMF itajadili maombi haya katika wiki zijazo.

"Uchumi wa Tanzania ulikua kwa asilimia 5.1 mwaka 2023 licha ya changamoto ya mgao wa umeme na uhaba wa fedha za kigeni hali iliyozorotesha shughuli za viwanda na biashara. Mfumuko wa bei wa asilimia 3.1 (mwaka hadi mwaka) mwezi Aprili 2024 umesalia ndani ya lengo la Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ingawa mfumuko wa bei ukiondoa bidhaa ya chakula ulipanda hadi asilimia 3.9 (mwaka hadi mwaka). Matarajio ni mazuri kutokana na ukuaji wa uchumi kutarajiwa kuongezeka hadi kufikia asilimia 5.4 mwaka 2024 ukisaidiwa na kuimarika kwa mazingira ya ufanyaji biashara na kupungua kwa bei za bidhaa duniani. Hatari kwenye matarajio haya zinaweza kutokana na kuongezeka kwa migogoro ya kikanda, mabadiriko kwenye bei za bidhaa duniani, kushuka ghafla kwa ukuaji wa uchumi duniani, kuendelea muda mrefu kuwepo kwa uhaba wa fedha za kigeni nchini, na kuongezeka kwa mafuriko kutoka na mvua za El Nino, ambavyo hivyo vinaweza kuathiri matarajio haya chanya.

“Nakisi ya mauzo na manunuzi ya bidhaa na huduma nje ya nchi mwaka huu wa fedha inatarajiwa kupungua hadi asilimia 4.3 ya Pato la Taifa, kutoka asilimia 6.5 Mwaka wa Fedha wa 2022/23. Hata hivyo, hali ya upatikanaji wa fedha za kigeni inatarajiwa kutokuwa nzuri hivyo shinikizo katika soko la fedha za kigeni huenda likaendelea. Benki Kuu ya Tanzania ilisisitiza dhamira yake ya kuruhusu mabadiliko zaidi kwenye viwango vya kubadilisha fedha za kigeni ili kufufua soko la fedha za kigeni baina ya mabenki na kuhakikisha viwango vya kubadilisha fedha vinaamuliwa na nguvu za soko, huku ikihakikisha inaingia tu kwenye soko inapojitokeza hali mbaya ya soko, kulingana na sera yake ya uingiaji sokoni. Benki Kuu ya Tanzania itachapisha matokeo ya minada yake ya fedha za kigeni ili kuongeza uwazi kwenye soko. Kuendeleza sera ya fedha ya kupunguza ujazi wa fedha kwenye uchumi kutasaidia pia juhudi za kupunguza shinikizo katika soko la fedha za kigeni na kuleta utulivu wa bei za bidhaa na huduma.

"Serikali inaendelea kutekeleza mpango wake wa kubana matumizi usioathiri ukuaji wa uchumi uliopo kwenye bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2023/24 huku ikilinda matumizi kwenye vipaumbele vya sekta za huduma za kijamii ikiwa ni pamoja na elimu, afya, na ulinzi wa kaya maskini. Juhudi hizi zinatarajiwa kuendelea katika Mwaka wa Fedha wa 2024/25, zikisaidiwa na sera ya kodi na juhudi za usimamizi wa mapato ya serikali ili kuongeza nafasi ya matumizi ya serikali. Mpango wa serikali wa mageuzi ya kimuundo unalenga kusaidia ukuaji wa uchumi thabiti, endelevu, na jumuishi unaotokana na kuboreshwa kwa mazingira ya kufanya biashara na utawala bora.

"Mpango wa RSF utasaidia juhudi za serikali katika kushughulikia changamoto za kisera kwenye masuala ya hali ya hewa na kutekeleza mageuzi ili kuimarisha uthabiti wa uchumi wa Tanzania. Serikali iko tayari kuimarisha utawala na uratibu wa sera zinazohusiana na mabadiliko ya tabia ya nchi kwa kuimarisha mfumo wa usimamizi wa maafa; kuingiza sera zinazohusiana na masuala ya mabadiliko ya tabia ya nchi katika bajeti na kwenye mipango ya uwekezaji wa umma; kuoanisha sera zinazohusiana na mabadiliko ya tabia ya nchi pamoja na sera na ahadi za kitaifa; na kuimarisha usimamizi wa sekta ya fedha kwa kuzingatia athari zitokanazo na mabadiriko ya tabia ya nchi. Mpango wa RSF utatoa rasilimali fedha za ziada zenye masharti nafuu ili kusaidia uwekezaji na kuharakisha utekelezaji wa mageuzi kwenye masuala ya tabia ya nchi na pia kuchochea ufadhili kwenye kukabiliana na mabadiliko tabia ya nchi.

"Ujumbe kutoka IMF ulikutana na Waziri wa Fedha, Mhe. Dr. Mwigulu Nchemba, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Mr. Emmanuel Tutuba, viongozi wengine waandamizi wa serikali, washirika wa maendeleo, na wawakilishi wa sekta binafsi. Wataalam kutoka IMF wanapenda kuzishukuru mamlaka za Tanzania kwa ushirikiano wao, ukarimu na majadiliano yenye tija."